TANGAZO LA SERIKALI NA. 130 la tarehe 21/2/2025

SHERIA YA USIMAMIZI NA TOZO YA USHURU
(SURA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MAWILI YA MRADI WA MFUMO WA IKOLOJIA NA UHIFADHI WA KATAVI – MAHALE WA HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Mawili ya Mradi wa Mfumo wa Ikolojia na Uhifadhi wa Katavi – Mahale wa Hifadhi za Taifa Tanzania ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanzakutumika kuanzia tarehe 13 Novemba, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuimarishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari mawili yaliyoainishwa kwenye Jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na kwa niaba ya Hifadhi za Taifa Tanzania kwa ajili ya Mradi wa Mfumo wa Ikolojia na Uhifadhi wa Katavi – Mahale kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia Ukomo tarehe 12 Machi, 2025.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Injini | Namba ya Chassis | Idadi | Eneo la Ununuzi Ndani ya Nchi/Nje ya Nchi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser 76 Hardtop 10 seater, 5 door | 1HZ-1076774 | JTEEB71 J80F031084 | 01 | Nje ya Nchi |
| 2 | Toyota Land Cruiser 76 Hardtop 10 seater, 5 door | 1HZ-1076868 | JTEEB71 JX0F031104 | 01 | Nje ya Nchi |

Dodoma,
30 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*